

Biblia inasemaje....

“Yesu aliyachukuliaje maandiko?”

Sehemu ya kwanza

Mafundisho yoyote ya nyakati za Biblia yataonyesha wanadamu kuwa Yesu alipokuwa duniani hakuwa na Agano Jipya likiwa limeandikwa. Walakini Yesu alikuwa na sehemu kubwa ya maandiko ya Agano la Kale. Kama leo tunataka kujua jinsi ya kuyachukulia maandiko, bila shaka tunapaswa kutazama kielelezo alichotuachia Yesu. Petro aliandika;

“Kwa sababu ndio mlioitwa; Maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuata nyayo zake” 1 Petro 2:21.

Yesu alipokuwapo hapa duniani, alituachia kielelezo jinsi tunavyotakiwa kuishi, kuabudu, kufundisha n.k. Na pia alituachia kielelezo jinsi tunavyotakiwa kuyachukulia maandiko. Watu wengi wa leo wanataka kuyatupilia mbali maandiko na kuyachukulia kama hadithi tu, huku wakiukana uweza wa milele ulio katika kila Neno la maandiko. Walakini, Yesu, mwana wa Mungu aliyaheshimu mno maandiko yaliyokuwepo nyakati za uhai wake duniani. Yesu alitambua kuwa yale maandiko yalikuwa ni pumzi ya Mungu katika Roho Mtakatifu.

Katika Marko 12, twaweza kusoma jinsi maadui wa Yesu walivyopanga kuushambulia ujumbe wa Yesu na mamlaka yake. Katika mstari wa 13, Mafarisayo na Maherode walijaribu “kumnasa katika maneno yake”. Baada ya kushindwa kumnasa Yesu, katika mstari wa 18 Masadukayo waliulipua mtego wakifuatiwa na mmoja wa waandishi (mstari wa 28,32). Waliposhindwa kumnasa, Yesu akajaribu kuwaonyesha maadui zake uwepo wake wa milele. Katika kuthibitisha asili yake ya milele, aliyanukuu maneno ya Daudi yaliyoko katika Zaburi 110:1, kwamba “yalinenwa na Roho Mtakatifu”